

**Dondoo za mkutano wa umma wa wapanda baiskeli Dar es Salaam
Tarehe 16 Septemba 2006**

Waliohuduria

Elaine Baker
Israel Kiyame
Juma Ali Salehe Jongo
Kibwana Mohammad Msiga
Maurus Malikita
Shukuru Hassan

Wageni

Godfrey Jax	CHABADA
Leon Mlambo	AALOCOM
Prosper Nyaki	AALOCOM
Saim Kengelle	CHABADA
Selemani Majembele	AALOCOM

Kabla ya mkutano huu, Elaine na Meja walikutana na Leoni Mlambo wa AALOCOM na Bradley Schroeder wa ITDP (Institute for Transportation and Development Policy). California Bike cooperative. Mkutano huu ulizalisha wazo la kuandaa msafara wa baiskeli.

Leon mlamba wa AALOCOM alieleza nia na malengo ya AALOCOM – (the Association for Advancement of low cost mobility) wamekuwa wakifanya kazi kusambaza baiskeli za califonia na wamesambaza zaidi ya 300. wamepanga kufanya utafiti jinsi baiskel zitakavyoinua kipato cha waliozipokea. Wanauza baiskeli kwa Tsh 120,000 kwa wwasambazaji ambao huziua kwa Tsh 140,000. wamekuwa wakifanya kazi na mashirika mengine katika nchi tofauti kusambaza baiskeli.

Mpango wa kufanya msafara wa baiskeli ulijadiliwa uchaguzi wa kutumia mnazi mmoja au karamjee kama mwanzo wa mwisho wa baiskeli ulijadiliwa. Karamjee aliamuliwa itumike. Tayari AALOCOM wameungwa mkono na msaidizi wa meya wa Dar es salaam atakayehudhuria kama mgeni maalumu na aliyetoa karamjee kama sehemu ya kukutana.

Njia za kupitia zilijadiliwa. Njia ya kwanza ilipendekezwa kuwa kutoka karamjee hadi Kivukoni , Sokoine, Msimbazi , barabara za UN na ocean. Godfrey CHABADA alishauri kwamba kufanya mzunguko kinyume ni vyema kwa sababu ya mfumo wa kuendeshea gari kushoto. Njia ilibadilishwa kuwa Nyerere na samora badala ya sokoine. Ilijadiliwa kwamba njia zitumike zile zenye watu wengi ili kuongeza uwezekano wa watu wengi kuona tukio hilo.

Matangazo yalijadiliwa. AALOCOM aliandaa nyaraka kuhusu msafara. Ilikubalika kutumia kurasa za mwisho za nyaraka hizo kwa matangazo. Elaine alisema atatengeneza mabango na vipeperushi na kuvipitisha kwa maoni. Ilikubalika kuweka nembo za mashirika yote matatu kwenye matangazo ambayo pia yataelezea kwamba wanawake , watoto, wanaume na vijana wanakaribishwa pamoja na aina zote za baiskeli (guta , na za walemavu) Itajwe kwamba ushiriki ni bure.

Ilisemekana kwamba itakuwa vizuri ikiwa tukio lenyewe litapambwa, kwa muziki na kwamba washiriki waambiwe kupamba baiskeli zao. Suala la T- shirt lilikataliwa kwani nigharama, zingeonyeshwa nembo ya mfadhili, tukio lingeonekana kama linalotangaza shirika zaidi.

Ilijadiliwa pia kuhusu tarehe. Tarehe 7 octoba ilipendekezwa hata hivyo hii ililandana na mbio za baiskeli shinyanga hivyo CHABADA hawatakuwepo. Tarehe 14 octoba ilipendekezwa na leoni alisema angejadili. Na msaidizi wa meya kujua kama atakuwepo na angetujulisha baada ya siku chache.

AALOCOM walisema IIDP wako tayari kutoa baiskeli 10 kwa bahati nasibu.

Israeli na malikita walisema wako tayari kuandaa kazi za kisanii kwa tukio hilo.

Ilikubalika kwamba tutakutana tena makundi yote wiki ijayo jumamosi sehemu hii na muda huu.